JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb.NA.AC/18/214/71** **26/01/2024**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KUJITOLEA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale anakaribisha maombi ya ajira ya kujitolea kwa kada za **Tabibu**, **uuguzi, Wataalam wa Maabara**, na **Mtaalam wa Mionzi** hii ni kutokana na program ya **COMMUNITY SOCIAL RESPONSIBILITY (CSR)** inayotolewa na Mgodi wa Uchimbaji Dhahabu wa Barrick Bulyanhulu kama ifuatavyo;

**1.TABIBU (Nafasi 04)**

**(A)SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa wenye Stahada ya Tabibu miaka mitatu (03) (Clinical Officer ) pia ambao wamesajiliwa na mabaraza pale inapohusika.

**(B) KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kutoa huduma za kinga na tiba

ii. Kutambua na kutibu magonjwa ya binadamu

iii. Kutoa huduma ya Afya ya Msingi (Primary Health care)

iv. Kufanya kazi atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, afya , uzoefu na ujuzi wake.

**2. MUUGUZI II (NAFASI 05)**

**(A) SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa wanye cheti cha uuguzi cha miaka miwili (02) kutoka katika chuo kinachotambuliwa na serikali kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la wauguzi na wakunga Tanzania.

**(B) KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, Hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za Afya.
ii. Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa Afya katika sehemu yake ya kazi.
iii. Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi.
iv. Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani.
v. Kutoa ushauri nasaha.
vi. Kutoa huduma za Kinga na uzazi wa mpango.
vii. Kutoa huduma za uzazi na Afya ya Mtoto.
viii. Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
ix. Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi
x. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana Elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**3. Mteknolojia Msaidizi - Maabara (Lab Assistant) (Nafasi 02)**

**(A)SIFA ZA MUOMBAJI**

Kuajiriwa wenye Astashahda katika fani ya uteknolojia ya muda wa miaka miwili (02) katika fani ya uteknolojia maabara katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikari na ambao wamesajiliwa na mabaraza pale inapohusika.

**(B) KAZI NA MAJUKUMU**

i. Kupima sampuli zinaletwa maabara.

ii. Kuhifadhi sampuli zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi au kupelekwa maabara za ngazi za juu.

iii. Kufanya kazi za ukaguzi wa maabara, vifaa, kemikali na hifadhi ya kemikali.

iv.Kuweka kumbukumbu za maabara ambazo zimepatikana wakati wa uchunguzi.

v.Kufundisha watumishi walio chini yake.

vi.Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**4. Mteknolojia Daraja II – Radiografa – (Nafasi 1)**

**(A) SIFA ZA MWOMBAJI.**

Kuajiriwa wenye stashahada katika fani ya uteknolojia ya muda wa miaka miwili (03) katika fani ya Radiolojia na mionzi katika vyuo vinavyotambuliwa na selikali na ambao wamesajiliwa na mabaraza pale inapohusika.

**(B) KAZI NA MAJUKUMU.**

i.Kuwapima wagonjwa wanaoelekezwa kwenye eneo lake la kazi.

ii.Kutunza mitambo na vifaa vya Radiolojia katika eneo lake la kazi.

iii.Kukagua picha za X-Ray zilizopimwa kwa ubora na kutosheleza (Diagnostic quality).

iv.Kutunza picha za wagonjwa hadi majibu yanapowafikia madaktari waliowatuma wagonjwa.

v.Kutoa ushauri kuhusu masuala ya kazi za Radiolojia na Mionzi katika eneo lake la kazi.

vi.Kuandaa vifaa vya tiba/uchunguzi na kusimamia utakasaji vifaa katika eneo lake la kazi.

vii.Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lake la kazi.

viii.Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi.

**MASHARITI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE**

I. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45

II. Waombaji wote waabatishe Picha mbili ''Pasport size ''za hivi karibuni.

III. Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa, Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au kitambulisho cha mpiga kura au hati ya kusafiria

IV. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.

V. Waombaji waambatanishe vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
-Degree/Advanced Diploma /Diploma/Certificates
-Cheti cha Mtihani wa kidato cha IV na VI
-Vyeti vya kitaaluma (Professional certificates from respective boards)

VI. Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**

VII. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhiniwa na Mamlaka husika Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Baraza la Mitihani la Taifa, (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE)

VIII. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria

Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **11/02/2024, Muhimu**, kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu. Anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale,
S.L.P 352,
**NYANG'HWALE**

Husna Toni

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

**NYANG'HWALE**

MKURUGENZI MTENDAJI
S.L.P 352
NYANG'HWALE